JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

Simu: 026-2322129
Nukushi: 026-2322128
Tovuti: www.michezo.go.tz
Baruapepe: km@michezo.go.tz



Mji wa Serikali - Mtumba
Mtaa wa Michezo,
S. L. P. 25,
40481 DODOMA.

24 Novemba, 2026 - Dodoma

TAARIFA KWA UMMA

MAANDALIZI YA AFCON 2027 YAZIDI KUPIGA HATUA

Kesho tarehe 25 Novemba, 2026 Tanzania itakabidhi rasmi Ofisi za Sekretarieti ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Barani Afrika (CAF) kwa ajili ya kutumika kwa Makao Makuu ya Maandalizi ya Mashindano ya AFCON 2027.

Sherehe za makabidhiano hayo zitafanyika katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere (JNICC), jijini Dar es Salaam zilipo ofisi hizo kuanzia saa 3:00 asubuhi.

Tukio hilo pia litahusisha utiaji saini wa Mkataba wa udhamini wa matangazo kati ya Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) na Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), utakaoiwezesha Bodi hiyo kuwa mshirika rasmi wa mashindano hayo.

Sherehe hizo ni sehemu ya maendeleo ya maandalizi ya pamoja kati ya Tanzania, Kenya na Uganda katika kuandaa AFCON 2027, yatakayounganisha wadau na mashabiki wa soka barani Afrika huku yakiitangaza Afrika Mashariki duniani.

Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo inawaalika Wananchi wote kufuatilia matangazo ya tukio hilo kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

#AFCON2027 #Pamoja #EastAfrica #TotalEnergiesAFCON2027

Digitally Signed By Zaituni Mkwama
Tue Nov 24 15:16:46 EAT 2026

Zaituni Mkwama
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini